


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA WAZIRI MKUU- TAMISEMI
HALMASHAURI YA WILAYA YA MERU



SHULE YA SEKONDARI MAKIBA

S. L. P 13818

ARUSHA.

TAREHE

NAMBA ZA SIMU

- 1. Mkuu wa Shule: 0754279170/0658279170/ na 0784 279170 (Kwa WhatsApp)**
- 2. Makamu Mkuu wa Shule: 0748060064/0674159611**
- 3. Mwandamizi Taaluma: 0758348788/0782136408**
- 4. Mwandamizi Malezi: 0715028291/0758532968**

KUMB. NA. MKSS/KUJ/K5/2025-2026

Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi.....

S.L.P

YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MAKIBA KIDATO CHA TANO HALMASHAURI YA MERU MKOA WA ARUSHA MWAKA

- 1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao..... amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika shule hii kwa mwaka huu wa masomo Tahasusi ya i) PCM (ii) EGM (iii) CBG (iv) HGL (v) HKL (vi) HGK Hivyo nachukua fursa hii kukupongeza sana wewe na mwanao, hongereni sana'**

Shule ya sekondari Makiba ipo kitongoji cha Korona, Kijiji cha Makiba, Kata ya Makiba, Tarafa ya Mbuguni, Halmashauri ya Wilaya ya Meru, Kusini-Mashariki mwa Jiji la Arusha.

NAMNA YA KUFIKA MAKIBA SEKONDARI UKITOKEA MJINI ARUSHA.

Kwa wanaotokea **Mkoa wa Arusha**, naweza kufika Shule ya Sekondari Makiba kupitia Arusha Mjini-Kikatiti (Kilometa 32) kisha Kikatiti - Makiba (Kilometa 22). Pia unaweza kufika Shuleni kupitia Arusha-Tengeru-Mbuguni-Mirerani-Makiba, au Arusha-Uwanja wa Ndege wa Kimataifa Kilimanjaro (KIA) Stand (Kilometa 45) kisha KIA Stand - Mirerani (Kilometa 30) kisha Mirerani-Makiba (Kilometa 4.5).

Kwa wanaotokea maeneo mengine mfano, **Dsm, Pwani, Morogoro na Tanga** kupitia Mkoa wa Kilimanjaro, utafika Makiba Sekondari kwa kutoka Manispaa ya Moshi-KIA Stand (Kilometa 35) kisha KIA Stand hadi Mererani na Mererani - Makiba (Kilometa 4.5).

- ↗ Kwa wale ambao wanatokea mikoa ya **Kanda ya Ziwa** kupitia Babati shuka kituo Kikuu cha mabasi Arusha Mjini kisha kupanda gari/kosta za Mirerani (nauli ni shilingi 4,000/=) na kisha kuchukua pikipiki kutoka Mirerani hadi Makiba Sekondari kwa shilingi 3,000/= au 4,000/=
- ↗ Kama utakosa gari la moja kwa moja kutoka Kituo Kikuu cha Mabasi Arusha Mjini hadi Mirerani unaweza ukapanda gari kutoka Kituo Kikuu cha Mabasi Arusha hadi Kikatiti kwa shilingi 1,500/= kisha ukapanda pikipiki hadi Makiba kwa shilingi 5,000/= au 6,000/= ama waweza kupanda gari kutoka Kituo Kikuu cha Mabasi Arusha hadi Standi ya KIA kwa shilingi 2000/= kisha upande daladala hadi Mirerani kwa shilingi 1,500/= kisha ukapanda pikipiki kutoka Mererani hadi Makiba Sekondari kwa shilingi 3,000/= au 4,000/=.
- ↗ Kwa wale wanaotokea mikoa ya Dar es Salaam, Morogoro, Tanga, Kilimanjaro kwa kupitia Moshi, watahukia kituo cha KIA kisha kupanda daladala kwenda Mirerani kwa shilingi 1500/= kisha watahukia kituo kinachoitwa Getini-Mirerani kisha kupanda daladala hadi Makiba kwa shilingi 3,000/= au 4,000/=.

Kwa maelezo zaidi Unaweza kuwasiliana kwa namba za simu zilizoandikwa hapo juu.

Muhula wa masomo utanza tarehe hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe kuanzia saa mbili asubuhi hadi saa kumi kamili jioni. Mwisho wa kuripoti ni tarehe saa kumi jioni.

2. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA NI: -

2.1 SARE ZA SHULE (SCHOOL UNIFORM)

- a) Mashati mawili (2) meupe yenye mikono mirefu yasiyo na maridadi (urembo) na yasiyoonesha ndani (non-transparent) na yasiyo ya kubana mwili.
- b) Suruali mbili (2) rangi ya **KAKI** yenye marinda mawili (2) (suruali mnyonyo haziruhusiwi kabisa ikikamatwa nayo itachanwa) na utalazimika kurudi nyumbani kushona nyingine
- c) Sweta rangi **NYEUSI**
- d) Tai rangi **NYEUSI** yenye michirizi myeupe iwe ndefu kiasi isizidi eneo la flaizi ya suruali.
- e) Sare za michezo ni Kaptura, Tisheti na Soksi rangi ya **KIJANI** ya CCM.
- f) Track suit ya rangi ya kijani yenye michirizi myeupe
- g) Viatu **VYEUSI VYA KUFUNGA NA KAMBA** vyenye visigino vifupi visivyo na urembo, vinapakwa rangi, viatu vyenye visigino virefu, visivyo na soli, ama vya plastic havitaruhusiwa shuleni. Atakaye kiuka atachukuliwa hatua za kinidhamu.
- h) Soksi **NYEUSI** jozi mbili
- i) Mkanda **MWEUSI** wa ngozi wa kuvalia suruali na usio na balkon kubwa isiyokuwa na picha yoyote.
- j) Nguo za kushindia (shamba dress) **Tisheti ya kijani shingo ya duara** isiyona maandishi yoyote na **suruali ya rangi nyeusi**.
- k) Tishet yenye nembo ya shule ya yakuvaa siku za masomo inapatikana kwenye maduka ya wafanya biashara yaliyo karibu na shuleni kwa shilingi 20,000/=

2.2. MICHANGO MUHIMU

- a) Michango inayotakiwa kulipwa na kila Mzazi/ Mlezi ni kama ifuatavyo:-

NA	AINA YA MICHANGO	KIASI
1	MCHANGO WA UENDESHAJI WA SHULE	65,000/=
2	TAHADHARI	5,000/=
3	NEMBO	5,000/=
4	KITAMBULISHO	5,000/=
	JUMLA	80,000/=

“MICHANGO YOTE ILIPWE KWENYE ACCOUNT YA SHULE, NMB A/C. NO. 40801200258 JINA LA A/C NI MAKIBA SECONDARY SCHOOL DEV- AC”.

(C) MAHITAJI YA LAZIMA KUIMARISHA TAALUMA UNAYOTAKIWA KUJA NAYO SHULENI.

- i. Ream (**isiyo na mistari**) mbili (2) kwa mwaka yaani rim moja kila mhula.
- ii. Ruled paper (**rim ya mistari**) mbili (2) kwa mwaka yaani moja kila mhula.

(D) MAAGIZO MUHIMU YA VITABU VYA KIADA NA ZIADA

ORODHA YA VITABU vifuatavyo hutumika kufundishia na kujifunzia katika shule za sekondari kwa kidato cha tano na sita. Kila mwanafunzi anatakiwa **KUNUNUA ANGALAU KITABU KIMOJA KWA KILA SOMO** kwenye Tahasusi husika yaani **PCM (Physics, Chemistry na Mathematics), EGM (Economics, Geography na Mathematics), CBG (Chemistry, Biology na Geography), HGL**

(History, Geography na English Language), HKL (History, Kiswahili na English Language) na HGK (History, Geography na Kiswahili).

Vitabu hivi ni kwa ajili kumsaidia mwanafunzi kwenye masomo yake binafsi.

1. VITABU VYA SOMO LA GENERAL STUDIES (GS).

- i. Understanding Advanced Level General Studies (2012) by Biligwamungu and Deogratus S.M
- ii. General Studies, Supplementary Book for Advanced Level and Colleges, 2nd Edition- Konrad Adenaker Stiftung

2. PHYSICS

- i. Principles of Physics by S. Chand Class XI & XII
- ii. Understanding Physics by Jim Breclhaupt
- iii. Advance Physics by Roger Munchester
- iv. Physics by Tom Duncan
- v. Calculation for A Level Physics
- vi. Physics ABBOT
- vii. Principle of Physics by M. Nelkon
- viii. Physics for Advanced Level Secondary Schools Student Book Form Five by Tanzania Institute of Education (TIE)
- ix. Physics for Advanced Level Secondary Schools Student Book Form Six by Tanzania Institute of Education (TIE)

3. CHEMISTRY

- i. Conceptual Chemistry by S. Chand, Class XI & XII
- ii. A Level Chemistry 4th Edition by EN Ramsden
- iii. Advanced Chemistry by Cambridge Low Price Edition Philip Mathew
- iv. General Chemistry for Advanced Level Secondary Schools Student's Book Form Five and Six (2019) by Tanzania Institute of Education (TIE)
- v. Physical Chemistry for Advanced Level Secondary Schools Student's Book Form Five and Six (2019) by Tanzania Institute of Education (TIE)
- vi. Organic Chemistry-A. Abdullah et al. A-Level and 1st Year Undergraduate Students Vol. III Part A.
- vii. Organic Chemistry-A. Abdullah et al. A-Level and 1st Year Undergraduate Students Vol. III Part B.
- viii. Organic Chemistry for Advanced Level Secondary Schools Student's Book Form Five and Six (2019) by Tanzania Institute of Education (TIE)
- ix. Inorganic Chemistry Part A.- J.S. Maro
- x. Inorganic Chemistry Part B.- J.S. Maro
- xi. Inorganic Chemistry for Advanced Level Secondary Schools Student's Book Form Five and Six (2019) by Tanzania Institute of Education (TIE)

4. BIOLOGY

- i. Biological Science; Cambridge University Press (1997) 3rd Edition
- ii. New Understanding Biology for A level by Susan Toole & G. Tool
- iii. Biology: A Functional Approach by B.M. V Roberts
- iv. Advance Biology Principles and Application by CJ Clegg and Mackean
- v. Advanced Biology by Michael Kent (2000).Oxford University Press UK

5. BASIC APPLIED MATHEMATICS (BAM) – FOR CBG STUDENTS

- i. Basic Applied Mathematics form 5 and 6 by Tanzania Institute of Education (TIE)
- ii. Basic Applied Mathematics for Form 5 and 6 by Kiza and Septine I Sillem

6. ADVANCED MATHEMATICS - PCM

- i. Pure Mathematics by K.J Backhouse (1 & 2)
- ii. Advanced Level Mathematics Volume 1 by L.K. Shayo
- iii. Engineering Mathematics by John Bird
- iv. Advanced Mathematics for Class XI & XII by S. CHAND
- v. Advanced Level Pure Mathematics, 4th Edition by C.J Tranta
- vi. Advanced Mathematics form 5 and 6 by Tanzania Institute of Education (TIE)

7. ECONOMICS

- i. Micro Economics for Advanced Secondary Schools (2022) by Tanzania Institute of Education (TIE)
- ii. Essential for A-Level Economics Paper 1, Abros Odhiambo

8. GEOGRAPHY

- i. Landform in Africa by Colin Bucle
- ii. Principles of Physical Geography (1975) by F. Monkhouse
- iii. Geography Integrated Approach by Waugh
- iv. Practical Geography for Africa by J. M Pritchard
- v. Human and Economic Geography by Morgan
- vi. A Comprehensive Approach to Physical Geography for Secondary School by D.T Msabila
- vii. A Integrated Regional Studies on Human and Economic Geography.Advanced Level paper 2, D.T Msabila
- viii. Photography Interpretation and Elementary Surveying for Secondary Level, New Edition-Dura
- ix. Tropical Lands by Michael Senior
- x. The Essentials of Practical Geography for Advanced Level by Joseph William Njiku (2005)
- xi. Practical Geography by Zisti Kamili

9. HISTORY

- i. Essentials in Advanced Levels History Paper 1 and Paper 2 by Saleh Yassin
- ii. History 1 and 2 by Bakari Madaya
- iii. Contemporary History Events by Shibitali C.K Tumaini
- iv. The Political Economy, Imperialism by Nabudere
- v. Mastering Advanced Level History Book II by Kato
- vi. Essentials in Advanced Level History Paper One, Paper Two by Saleh Yassin

10. ENGLISH

- i. Advanced Level English Language 1 form 5 and 6 by Ndambo S and Kinunda J
- ii. English for Advanced Level Secondary Schools Form 5 and 6 by Tanzania Institute of Education (TIE)
- iii. English Language for Advanced Level by Shaban Shafii
- iv. Advanced Level English Competence Based Approach by Nicholas Asheli
- v. English Language for secondary school, Literature & stylistics for form v & vi.
- vi. Advanced Level Literature by Asheri, N.

(b) PLAY/DRAMA

- i. An Enemy of the People by H. Ibsen
- ii. I Will Marry When I want by Ngugi wa Thiong'o
- iii. Lwanda Magere by Okot Omtatah -1991
- iv. The Beautiful Ones Are Not Yet Born by Ayi Kwei Armah.
- v. A Man of the People by Chinua Achebe.
- vi. Divine Providence by Severin N. Ndunguru.
- vii. His Excellence Head of State by Danny Safo.
- viii. Betrayal in the City by Francis Imbunga
- ix. An Enemy of the People by John Ruganda

(c) POETRY

- i. Selected Poems by Tanzania Institute of Education (TIE)
- ii. The Wonderful Surgeon and other Poems by Charles Mloka.

(d) NOVELS AND SHORT STORIES (aje na vitabu viwili kati ya hivyo)

- i. The Beautiful Ones Are Not Yet Born by Ayi Kwei Armah.
- ii. A Man of the People by Chinua Achebe.
- iii. Divine Providence by Severin N. Ndunguru.
- iv. His Excellence Head of State by Danny Safo.
- v. Encounters from Africa by Macmillan Education Limited.

11. KISWAHILI

(a) USHAIRI

- i. Kimbunga by G. Gora (Tasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili) 1999
- ii. Chungu Tamu by T.A Mvungi (Tanzania Publish House) 1985
- iii. Mapenzi Bora by Shaban Robert (Mkuki na Nyota) 2003
- iv. Fungate ya Uhuru by S.M Khatibu

(b) RIWAYA

- i. Vuta nikuvute by A. Shafii (Mkuki na Nyota) – 1999
- ii. Mfadhili by Hussein Tuwa
- iii. Usiku utakapokwisha by Mbunda Msokile

(c) TAMTHILIA

- i. Moran by E. Mbogo
- ii. Kivuli Kinachoishi by Said Mohamed -2007
- iii. Kwenye Ukingo wa Thim by E. Hussein
- iv. Nguzo Mama 1982

(e) MAHITAJI MENGINE

- i. Dissecting kit kwa wanafunzi wa Biology
- ii. Scientific calculator
- iii. Laboratory coat kwa wanafunzi wa tahasusi za CBG na PCM
- iv. Mathematical set, kalamu za wino (bluu/nyeusi ball pens za kutosha), penseli na vifaa vingine vya kujifunzia
- v. Madaftari (counter books za kutosha masomo 10)
- vi. Majalada (File cover) mawili ya plastiki kwa ajili ya kufungulia faili na kutunzia mitihani na majaribio
- vii. Picha za Passport size 2
- viii. Kamusi kubwa ya Kingereza (Dictionary) kati ya Oxford au Cambridge
- ix. Kamusi kubwa ya Kiswahili kwa wanafunzi wa tahasusi za HKL na HGK
- x. Begi au mfuko mzuri wa kuwekea vifaa vya shule
- xi. Sanduku imara la kuhifadhi mali zako. Tutapokea sanduku moja tu la chuma ‘TRANKA’
- xii. Mahitaji yote ya bafuni mafano sabuni, mafuta, msawaki, taulo nk
- xiii. Godoro futi 3 kwa 6
- xiv. Mashuka pair 2, foronya 1 (vyote hivi rangi ya bluu bahari), blanketi 1 na chandarua 1 rangi yoyote vyote viwili.
- xv. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe)
- xvi. Ndoo ndogo mbili zenye mifuniko
- xvii. Kwanja 1, jembe 1, hard bloom, fagio (chelewa), mopa na skuiza kwa ajili ya usafi
- xviii. Ulete result slip nakala halisi pamoja na nakala kivuli moja (original and copy) shuleni

Kaulimbiu ya shule yetu ni: ‘MBELE DAIMA NYUMA MWIKO’

Lengo letu ni kumjenga mwanafunzi kuwa na mwenendo mzuri na hivyo kumwezesha kufanikisha lengo la alichokifuata hapa. Sheria hizi zitasaidia kuleta hali ya AMANI/UTULIVU; MSHIKA/UMOJA na FURAHA shuleni na kumfanya kuwa raia bora na mwema. Kila mwanafunzi aje akiwa na nia ya KUSOMA KWA BIDII na ajitahidi kuishi vizuri na wenzake hapa MAKIBA SEKONDARI.

Kwa upande wa shule, sisi WALIMU pamoja na WAFANYAKAZI WASIO WALIMU tutajitahidi kuishi, kumfundisha na kumlea mtoto lakini tutashindwa katika kazi hii bila ushirikiano mzuri wa wazazi/walezi, hivyo tunatoa rai kwa wazazi au walezi kushirikiana kwa karibu.

Vifuatavyo ni vifungu muhimu vya **SHERIA ZA SHULE**. Kila mwanafunzi anapaswa kuzizifuata sheria hizi kikamilifu.

- ↗ Lugha inayotumika darasani (katika kufunza na kujifunza) na nje ya darasa yaani (kwa mawasiliano ya siku kwa siku) ni lugha ya kiingereza pekee. Hii itasaidia kuleta ufanisi katika kumudu stadi za kufunza na kujifunza masomo mbalimbali.
- ↗ Kwa vile shuleni ni mahali pa kusoma inatakiwa pawe na ukimya hasa sehemu za madarasani
- ↗ Kila mwanafunzi ni lazima ahudhurie vipindi vyote vinavyompasa kama ratiba kuu ya shule inavyoonesha.
- ↗ Kazi za mikono ni moja ya elimu inayotolewa hapa shuleni hivyo kila mwanafunzi hana budi kushiriki kikamilifu bila kutegea.
- ↗ Hairuhusiwi kupeleka chakula nje ya bwalo la chakula kama bwenini. Wagonjwa watapelekewa chakula kwa kufuata taratibu zilizowekwa
- ↗ Mwanafunzi haruhusiwi kuleta chakula cha aina yoyote pindi arudipo shuleni toka likizo au arejeapo baada ya kupata kibali kutoka ndani ya shule.
- ↗ Mavazi yote ya binafsi hayahitajiki shuleni. Mwanafunzi atalazimika kuvaa sare na nguo za kushindia tu (shamba dress) isipokuwa muda wa michezo ambapo atavaa sare za michezo.
- ↗ Mwanafunzi haruhusiwi kukaa na dawa za aina yoyote bwenini. Kwa mwanafunzi mwenye dawa atoe taarifa kwa Patroni ili ziweze kuhifadhiwa na kuzitumia kwa utaratibu.
- ↗ Wanafunzi hawaruhusiwi kupeana dawa bwenini.
- ↗ Mwanafunzi haruhusiwi kuwa na vyombo vya kielekitroniki, mfano simu, vifaa vya muziki kama vile redio, Walkman, earphone na headphone, kamera n.k
- ↗ Mwanafunzi haruhusiwi kuwa na simu/ laini ya simu, au hata kuhifadhi simu nje ya shule.
- ↗ Wizi, matusi na ugomvi haviruhusiwi kabisa iwe ni ndani au nje ya shule.
- ↗ Mwanafunzi haruhusiwi kumiliki silaha ama kuwa na vitu vya hatari vya ncha kali kama vile visu, nondo, nyundo, rungu, n.k
- ↗ Kila mmoja anawajibika kuvitunza vifaa vyote vya shule atakavyo kabidhiwa na asivyokabidhiwa kwa uangalifu wa hali ya juu.
- ↗ Uharibifu au upotevu wowote utakaotokea, gharama za matengenezo au fidia zitalipwa na atakayefanya uharibifu huo au kwa ujumla wa. Kila mmoja ni mlinzi wa mali za umma.
- ↗ Kila IJUMAA, JUMAMOSI na JUMAPILI wale waendao kusali kwenye madhehebu mbalimbali watavaa sare za shule na kurudi baada ya sala zao kukamilika
- ↗ Kila mwanafunzi anatakiwa kuheshimu watu wote hapa shuleni pamoja na uongozi wa shule na uongozi wa wanafunzi, kila mmoja ni lazima atumie lugha safi kwa watu wote na atatoa matatizo yake kwa viongozi wake kwa kufuata utaratibu uliopangwa/ kufuata ngazi.
- ↗ Ni **marufuku mwanafunzi kwenda nje** ya shule ama kwenye nyumba za walimu/wafanyakazi wa shule bila kibali.
- ↗ Mwanafunzi ataenda kununua mahitaji kwenye duka la shule mudawa mapumziko tu.

3. MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE

- i. Wizi
- ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro
- iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo
- iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla
- v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga Mwalimu ama mtu yeyote yule
- vi. Kufuga ndevu
- vii. Ulevi ama unywaji wa pombe na mwaumizi ya madawa ya kulevya
- viii. Uvutaji wa sigara
- ix. Uasherati; Ushoga; Uhusiano wa jinsi moja; Usagaji; kuo au kuolewa.
- x. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi
- xi. Kusababisha mimba/ujauzito ama kumpa mimba msichana
- xii. Kutembelea nyumba za starehe ama nyumba za kulala wageni
- xiii. Kumiliki, kukutwa ama kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule
- xiv. Kudharau bendera ya Taifa na Wimbo wa Taifa
- xv. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kamaa kunywa sumu nk
- xvi. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi

4. Viambatanisho na Fomu Muhimu

- a) Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa hospitali ya Serikali – vituo vya Afya, hospitali mfano za Wilaya au Mkoa.
- b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/ mkataba wa kutoshiriki katika mgomo, fujo na makosa ya jinai.
- c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni kulipa ada, michango na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.
- d) Michoro ya muonekano wa mavazi/sare za shule jinsi zitakavyoshonwa.
- e) Picha nne za passport size za hivi karibuni za mwanafunzi husika.

Tafadhali soma kwa makini maelezo/ maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

KARIBU SANA KATIKA SHULE YETU YA MAKIBA SEKONDARI.


MUHIMU.

KUMBUKA - Mwanafunzi akija na simu wakati wa “KURIPOTI KWA MARA YA KWNZA” akifika atakabidhi simu yake Ofisi ya Mkuu wa Shule na atarudishiwa wakati wa kurejea nyumbani. Yaani hapaswi kuja na simu na kuitunza/ kuificha popote pale kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayerusiwa kutunza simu ya mwanafunzi.

TAHADHARI: NGUO ZOZOTE ZA NYUMBANI nje na zilizoelekezwa hapo juu HAZIRUHUSIWI SHULENI ukikamatwa nayo/ nazo ITACHOMWA /ZITACHOMWA MOTO

Saini ya Mkuu wa Shule

Jina la Mkuu wa Shule.....



Mhuri wa Mkuu wa Shule

FOMU YA KUKUBALI NAFASI NA UTII

Mimi..... (jina kamili)

Kidato cha..... Mwaka

Nakubali na nina ahidi kufuata sheria, kanuni na taratibu zote za shule kama zilivyopangwa. Endapo nitaenda kinyume cha sheria, kanuni na taratibu za shule ninakubali nichukuliwe hatua za kinidhamu.

Tarehe

Jina na sahihi ya Mwanafunzi

Tarehe

Sahihi ya Mkuu wa Shule


FOMU HII INASAINIWA NA MWANAFUNZI TAJWA HAPO JUU IKISHUHUDIWA NA

Mimi Mzazi/ Mlezi wa nimesoma na kuelewa /kukubaliana na sheri na kanuni za shule. Endapo mtoto wangu atashindwa kufuata hayo yote hatua kali dhidi yake zichukuliwe ikiwa ni pamoja na kusimamishwa masomo na ikibidi kufukuzwa shule.

Tarehe Jina na sahihi ya Mzazi/ Mlezi.....

Tarehe Jina na sahihi ya shahidi.....

Tarehe Sahihi na Mhuri wa Mkuu wa shule



**PRIME MINISTER'S OFFICE
REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT
MAKIBA SECONDARY SCHOOL
MEDICAL EXAMINATION FORM**

To be Completed by Medical Officer in a Government Hospital in respect of all new entrants to Makiba Secondary School.

Full name -----

Age: -----

1. "AIDS" Test -----

2. Blood count (red & white) -----

3. Urine examination -----

4. Stool examination -----

5. Syphilis test -----

6. T.B Test -----

7. Ear Test -----

8. Eye Test -----

9. Spleen Test -----

10. Abdomen Test -----

11. Additional information or any other physical, mental, hereditary or intoxication diseases.

(Please state nature of treatment)

.....

I certify that the above mentioned has been examined and found it to/ not to pursue further education.

Signature -----

Designation -----

Station -----

Date: -----

Official stamp -----